

MOBILEMONEYOPERATOR Money Wezesha Training Script

Habari gani. Hapa ni MOBILEMONEYOPERATOR. Tumeanzisha mradi mpya uitwao MOBILEMONEYOPERATOR Money Wezesha. Nia na madhumuni ya MOBILEMONEYOPERATOR Money Wezesha ni kukupatia taarifa zitakazokuwezesha kufanya maamuzi mazuri zaidi kuhusu kiasi cha pesa unacho kuwa nacho unapoanza siku. Hii itaweza kuboresha kiasi cha float au salio kabla ya kuongeza salio lako kwa njia ya ASR au kupitia benki yako asubuhi.

MOBILEMONEYOPERATOR Money Wezesha ni matokeo ya utafiti wa kina sana. Tumeangalia kwa umakini taarifa za miamala ya mawakala wote. Tumegundua kuwa mawakala wengi huishiwa salio kwa sababu aidha hawana salio lolote la pesa talimu au kwa sababu hawakufanya shughuli zao kwa kuzingatia bajeti. Kwa kuchambua historia yako ya miamala, tutaweza kukupatia taarifa makhsusi kwa ajili yako zitakazokuwezesha kuongeza kiasi cha kamisheni zako.

MOBILEMONEYOPERATOR Money Wezesha hutoa mapendekezo ya kiasi gani cha float na pesa taslimu unapaswa kubeba unapotaka kusawazisha salio lako. Pia tunapiga hesabu kuwa ni kiasi gani cha pesa unaingiza na kutoa kwenye biashara yako ndani ya siku ya kawaida na siku yenye shughuli nyingi kuliko kawaida. Kuanzia tarehe 22 Agosti 2016, na kuendelea, kwa muda wa wiki nne, unaweza kupokea kati ya mapendekezo au taarifa au ukapokea yote mapendekezo na taarifa kuhusu miamala yako kila ifikapo jioni. Na kuanzia tarehe 19 Septemba 2016, na kuendelea kwa wiki nne, utapokea yote mapendekezo na taarifa kuhusu miamala yako kila ifikapo jioni.

Sio kila wakala atakayepokea SMS hizi. Hizi taarifa ni makhsusi na zinategemeana na historia yako binafsi ya miamala ndani ya biashara yako- pendekezo au taarifa itakayoletwa kwako haitokuwa na manufaa kwa wakala yeyote yule mwingine ambaye miamala yake ni tofauti na ile ya kwako kwa siku. Tafadhali usionyeshe taarifa na mapendekezo utakayopokea kwa mtu yeyote mwingine kwani hii haitokusaidia wewe wala biashara yako na inaweza kumweka hatiani utakayemshirikisha.

Mapendekezo na taarifa utakazopokea kupitia MOBILEMONEYOPERATOR Money Wezesha ndani ya hizi wiki nane zijazo zinaweza kutumika kufanya maamuzi bora zaidi na kukuwezesha kutengeneza faida kubwa zaidi. Kiwango sahihi cha float na salio la pesa taslimu kwa ajili yako kitategemea na kiasi cha wateja unaopata na wingi wa miamala inayofanyika kwenye biashara yako siku hadi siku.

Mtiririko wa wateja wako wanapofika kwako kila siku ni muhimu kwani pesa zinazotoka zinakata pesa zinazolingia. Kwa ujumla, unahitaji bajeti iliyo chini ya kiwango cha ujumla wa miamala yako. Lakini, iwapo miamala mingi ya kupokea na kutoa pesa inayofanana kwa viwango vya utoaji na upokeaji, au kama miamala ya kupokea ni mingi kuliko ya kutoa, hapo utahitaji kuwa na bajeti kubwa Zaidi.

Pili, ughafla- huwezi kujua ni kiasi gani cha wateja utaweza kupata kila siku. Ukibaki na mkakati wa kima cha chini, ipo siku utapata faida kubwa na ipo siku utapata faida ndogo. Hili halina neno ilimradi unahakikisha unapata muendelezo wa siku zenye faida kwa kipindi kirefu. Faida ya kila siku sio jambo la uhakika ila lenga kuwa na jumla ya faida ya mwezi iliyopo juu iwezekanavyo.

Asante kwa kusikiliza ujumbe huu kuhusu MOBILEMONEYOPERATOR Money Wezesha. Ni matumaini yetu kuwa utakuwezesha kuuelewa vema mkakati wetu.